MSWADA
WA
KUANZISHA SHERIA YA KUPUNGUZA NA KUKABILIANA NA MAAFA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, 2015, na itaanza kutumika kwa tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi.

kusomwa.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Dharura" maana yake ni tukio linalojumuisha athari ndogo ndogo kwa jamii ambazo zinaweza kusimamiwa vizuri kwa kutumia rasilimali za jamii hiyo;

"Kamati" maana yake ni Kamati za Kitaalamu, Wilaya na Shehia za Kukabiliana na Maafa Zanzibar zilizoanzishwa kwa mujibu wa Vifungu vya 11, 13, 16 na 19 vya Sheria hii;

"Kamisheni" maana yake ni Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Kujiandaa na Maafa" maana yake ni hatua za awali na taratibu zinazochukuliwa katika kupunguza na kukabiliana na mambo yanayosababisha maafa kwa kufanya uchambuzi wa athari ili kupunguza vifo na upotevu wa mali, hatua hizo ni pamoja na kuiandaa jamii, kutoa mafunzo, kuandaa mipango, vifaa, ramani za majanga, hifadhi ya mali na taarifa kwa umma

"Kujikinga na Maafa" maana yake ni hatua zinazochukuliwa katika kujikinga na majanga ya asili au yanayotarajiwa kutokea kutokana na athari mbaya kwa watu au uchumi;

"Kukabili maafa" maana yake ni utoaji wa huduma za dharura na misaada kwa umma wakati na mara baada ya matukio ya maafa kwa lengo la kuokoa maisha, kupunguza athari za kiafya, kuhakikisha usalama kwa jamii na kutoa huduma muhimu kwa walioathirika;

"Kukabiliana na Maafa" maana yake ni utaratibu maalum wa kutumia miongozo ya kiutawala, taasisi na kwa kutumia ujuzi

na uwezo wa kutekeleza mikakati, sera na kuimarisha uwezo kwa lengo la kupunguza athari za majanga na maafa;

"Kupunguza athari za Maafa" maana yake ni hatua zinazochukuliwa kupunguza athari za majanga ya kimaumbile, uharibufu wa mazingira, majanga ya kiteknolojia na kuhakikisha jamii zilizo katika hatari zina uwezo wa kukabili na kupunguza za maafa;

"Kupunguza vihatarishi vya maafa" maana yake ni dhana na utekelezaji wa kupunguza mambo yanayosabisha maafa kwa kufanya uchambuzi na kudhibiti visababishi vya maafa, ikiwa ni pamoja na kupunguza uwezekano wa kutokea majanga, uwezekano wa kuathiriwa kwa watu na mali, usimamizi mzuri wa ardhi na mazingira na kuimarisha maandalizi kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya majanga na maafa;

"Kurejesha hali baada ya maafa" maana yake ni hatua zinazochukuliwa mara tu baada ya kutokea athari za maafa ili kuirejesha jamii katika hali yake ya kawaida;

"Maafa ya Kimaumbile"maana yake ni maafa yanayotokana na matukio ya kimaumbile yanayojumuisha matetemeko na maporomoko ya ardhi, sunami, pepo kali, kudidimia kwa ardhi, vimbunga, mafuriko, ukame, moto na miripuko ya maradhi;

"Maafa yanayosababishwa na binadamu" maana yake ni maafa yanayotokana na shughuli za binadamu zinazojumuisha migogoro ya kijamii, vurugu, uchafuzi wa mazingira, vita, uharamia, ugaidi, umwagikaji wa mafuta, miripuko ya moto, mafuriko, maradhi ya mripuko, kuzama na kuporomoka kwa majengo, kukatika kwa umeme, ajali za viwanda pamoja na ajali zinazotokana na vyombo vya usafiri;

"Maafa" maana yake ni tukio kubwa linalotokea na kuathiri utaratibu wa maisha ya jamii na kusababisha madhara makubwa kwa watu, mali, uchumi na mazingira ambalo huzidi uwezo wa jamii kuweza kukabiliana nalo kwa kutumia rasilimali walizonazo;

"Majanga ya Kimaumbile" maana yake ni tishio linalotokea kimaumbile ambalo husababisha athari mbaya kwa watu au mazingira;

"Majanga" maana yake ni matukio ya hatari, vitu, shughuli za binadamu au hali inayoweza kusababisha upotevu wa maisha,

majeraha au athari nyengine za kiafya, uharibifu wa mali, huduma za kijamii, uchumi au mazingira;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Kukabiliana na Maafa wa Zanzibar unaoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni anayeteuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria hii;

"Mtu" maana yake ni mtu ambaye ama anafanya kazi katika Serikali au binafsi, au kikundi cha watu, jamii, taasisi ya Serikali au shirika;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Vihatarishi" maana yake ni mambo yanayoweza kusababisha uharibifu, madhara, hasara, upotevu au matukio mengine hatarishi ambayo yanaweza kuepukwa kwa kuwepo maandalizi ya mapema; na

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na uratibu wa kukabiliana na maafa.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KAMISHENI

Kuanzishwa kwa Kamisheni
Vifungu vipya 8A,8B na 8C

3.(1) Kuanzishwa Kamisheni ambayo itajulikana kama Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ambayo itahusika na kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa sera za Serikali kwa ajili ya kukabiliana na maafa.

(2) Kamisheni ni Wakala wa Serikali na itakuwa:

(a) endelevu na muhuri wake;

(b) na uwezo wa kununua, kukopa, kumiliki, kuuza mali inayohamishika na isiyohamishika kama ilivyoainishwa katika taratibu za manunuzi ya Serikali; na

(c) uwezo wa kutekeleza kazi ambazo Wakala anaweza kutekeleza kisheria.

(3) Kamisheni itakuwa ni chombo cha juu kinachotoa maamuzi yanayohusiana na kukabiliana na maafa Zanzibar na mambo yanayohusiana nayo.

Muundo wa Kamisheni.

4.(1) Kamisheni itakuwa chini ya uenyekiti waMakamu wa Pili wa Rais.

(2) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuwa Makamu Mwenyekiti.

(3) Wajumbe wa Kamisheni watakuwa:

(a) Mawaziri wote wa Serikali;

(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi;

(d) Wakuu wa Mikoa wa Zanzibar;

(e) Kamanda wa Brigedi ya Zanzibar, Jeshi la Wananchi la Tanzania;

(f) Kamishna wa Polisi, Zanzibar;

(g) Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, Zanzibar;

(h) Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM); na

(i) Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

(4) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na uratibu wa kukabiliana na maafa atakuwa Katibu wa Kamisheni.

Kazi za Kamisheni

5. Kamisheni itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuanzisha sera za kukabiliana na maafa, kanuni, mipango, mikakati na miongozo ili kuweza kukabiliana na maafa kwa wakati na kwa ufanisi;

(b) kuwezesha upatikanaji wa fedha na rasilimali nyengine wakati wa dharura au maafa;

(c) kusimamia utekelezajiwa mipango ya kukabiliana na maafa wakati wa maafa au dharura na kutoa miongozo na maelekezo yanayofaa katika utekelezaji wa mipango hiyo;

(d) kuratibu kazi za utoaji wa huduma na hatua za kujiandaa wakati wa maafa;

(e) kuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu kazi za kukabiliana na maafa;

(f) kupendekeza kwa Serikali juu ya utaratibu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na maafa;

(g) kuimarisha uwezo wa Serikali katika kusimamia matukio ya dharura na maafa;

(h) kutafuta rasilimali ndani na nje ya Zanzibar ili kuweza na kukabiliana na maafa kwa ufanisi;

(i) kuhakikisha uwepo wa uwajibikaji wa taasisi muhimu katika utekelezaji wa Sheria hii;

(j) kuhakikisha kuwa sera za Serikali, sheria, mipango na kazi za kukabiliana na maafa zinaendana na makubaliano na mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya kukabiliana na maafa;

(k) kuhakikisha kuwa Serikali kuu, Wilaya na Shehia zina uwezo wa kukabiliana na maafa kwa kuzipatia taaluma na vifaa; na

(l) kufanya kazi yoyote ambayo Kamisheni itaona inafaa kufanya katika mambo yanayohusiana na kukabiliana na maafa.

Uwezo wa Kamisheni

6. Kamisheni itakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuanzisha kikosi kazi, iwapo itaonekana inafaa, pamoja na kutoa miongozo itakayosaidia katika utekeleaji wa kazi za kukabiliana na maafa;

(b) kutafuta na kukusanya taarifa mbali mbali kutoka kwa mtu yeyote kwa madhumuni ya kusaidia shughuli za kukabiliana na maafa;

(c) kutumia ardhi, jengo au vifaa vyovyote na huduma kwa muda kwa lengo la kutekeleza kazi mbali mbali zinazohusiana na maafa;

(d) kutatua migongano yakitaasisi za Serikali katika kutekeleza kazi na majukumu yaokwa mujibu wa Sheria hii;

(e) kutoa maelekezo kwa Wizara, Idara, Wakala, Mkoa au Wilaya yoyote katika kutekeleza maamuzi ya Kamisheni katika mambo yanayohusiana na maafa;

(f) kumshtaki mtu yeyote ambaye amekataa kutoa au kupokea huduma wakati wa dharura au maafa; na

(g) kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika,kufanya ukaguzi kwa mtu yeyote, jengo, eneo au chombo kwa lengo la kukinga, kupunguza na kukabiliana na maafa na hali za dharura.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji

7. (1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu yoyote atafaa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa ni:

(a) Mzanzibari;

(b) mwenye angalau Shahada ya Kwanza ya fani inayohusiana na uongozi ; na

Afisa Mwandamizi wa Umma.

Sekretarieti ya Kamisheni

8. Kuanzishwa Sekretarieti ya Kamisheni ambayo itaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji.

Vitengo vya Sekretarieti

9. (1) Sekretarieti baada ya kushauriana naKamisheni na kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, itaanzisha Vitengo kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Kila Kitengo kitakuwa na Mkuu ambaye atapendekezwa na Mkurugenzi Mtendaji na kuidhinishwa na Kamisheni.

(3) Wakuu wa Vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Kazi za Sekretarieti

10. Sekretarieti itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuandaa na kufanya utetezi na kujenga uwezo katika ngazi zote ili kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa;

(b) kushajiisha uingizaji wa masuala ya kukabiliana na maafa katika mipango ya maendeleo, sekta, miradi, mikakati na mipango mengine ya kiutawala;

(c) kuandaa mpango wa mawasiliano na kujenga uwelewa kwa umma na wadau wengine kuhusu masuala ya kukabiliana na maafa;

(d) kuandaa ramani na kufanya tathmini ya kuainisha maeneo na vitu vilivyo katika hatariya kukumbwa na maafa na viwango vya hatari hizo;

(e) kuwezesha utoaji wa mafunzo na kufanya utafiti kuhusu masuala ya kukabiliana na maafakwa kushirikiana na wadau wengine pamoja na kutoa vifaa na nyenzomuhimu za kupunguza athari za maafa;

(f) kushirikiana na taasisi mbali mbali katika kuondoa vikwazo vinavyoweza kuzuia juhudi za kukabiliana na maafa;

(g) kuandaa na kuratibu vikao vyote vya Kamati ya Kitaalamu na Kamisheni;

(h) kuanzisha na kuziendeleza ghala za vifaa vya kukabiliana na maafa katika ngazi ya Taifa na Wilaya;

(i) kuandaa bajeti na mpango wa utekelezaji wa kazi za Kamisheni;

(j) kuandaa na kuwasilisha kwa Kamisheni ripoti ya utekelezaji ya mwaka;

(k) kushirikiana na taasissi zinazohusika kufanya ukaguzi na kusimamia majengo, vifaa, nyenzo ili kugundua mambo yanayoweza kusababisha maafa;

(l) kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamisheni;

(m) kutekelezakazi za kila siku na maamuzi yanayotolewa na Kamisheni;

(n) kukusanya na kuchambua takwimu za majanga na maafa na kuzisambaza kwa Wizara zote, Idara, Wakala na watu binafsi;

(o) kutengeneza na kutekeleza mfumo wa huduma za mawasiliano ya dharura kwa masaa ishirini na nne;

(p) kuviwezesha vituo vya uokozi vilivyopo katika maeneo tofauti kufanya kazi kwa ufasini;

(q) kuanzisha na kuendesha kituo kikuu cha tahadhari ya awali kwa lengo la kujiandaa na kukabiliana na maafa;

(r) kuweka na kuhifadhi kumbukumbu na taarifa zote zinazohisiana na maafa; na

(s)kutekeleza kazi yoyote kama itakavyoelekezwa na Kamisheni.

SEHEMU YA TATU
KUANZISHWA KAMATI

Kamati ya Kitaalamu

11. (1) Kunaanzishwa Kamati ya Kitaalamu ambayo itakuwa chini ya uenyekiti waKatibu Mkuu wa Wizara inayohusika na uratibu wa kukabiliana na maafa.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Kitaalamu watakuwa:

(a) Makatibu Wakuu wa Serikali;

(b) Naibu Mwanasheria Mkuu;

(c) Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Zanzibar;

(d) Afisa Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Polisi Zanzibar;

(e) Afisa Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Brigedi ya Zanzibar;

(f) Afisa Mkuu wa Utawala wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi;

(g) Afisa Mkuu wa Utawala wa Idara ya Usalama wa Taifa, Zanzibar;

(h) Afisa Mkuu wa Utawala wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM);

(i) Katibu Mtendaji Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar;

(j) Makatibu tawala wa Mikoa Zanzibar; na

(k) Wajumbe watatu wakuteuliwa na Waziri kutoka katika jumuiya zisizo za kiserikali, jumuiya za kijamii na taasisi nyengine siziso za kiserikali zinazohusika na kazi za kukabiliana na maafa baada ya kushauriana na taasisi husika.

(3) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa Katibu wa Kamati ya Kitaalamu.

Kazi za Kamati ya Kitaalamu

12. (1) Kamati ya Kitaalamu itakuwa na jukumu la kuishauri Kamisheni kuhusu mambo yote ya kukabiliana na maafa Zanzibar.

(2)Kamati ya Kitaalamu itatekeleza maelekezo yote yanayotolewa na Kamisheni.

Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

13. Kunaanzishwa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya katika kila Wilaya ya Zanzibar.

Muundo Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

14. (1) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya.

(2) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya;

(b) Meya wa Manispaa au Mwenyekiti wa Mji au Baraza la Wilaya;

(c) Afisa usalama wa Wilaya;

(d) Kamanda wa Polisi wa Wilaya;

(e) Kamanda wa Zoni wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania;

(f) Afisa wa Zoni wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM);

(g) Afisa wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi wa Wilaya;

(h) Kamanda wa Zoni wa Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ);

(i) Afisa Uhamiaji wa Wilaya;

(j) Afisa Afya wa Wilaya;

(k) Mwakilishi kutoka Jumuiya za Kiraia;

(l) Afisa Mipango wa Wilaya; na

(m) Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Wilaya husika.

(3) Afisa anayehusika na kukabiliana na maafa wa Wilaya atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

Kazi za Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

15. (1) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia programu za kukabiliana na maafa na utekelezaji wake katika ngazi ya Wilaya;

(b) bila ya kuathiri masharti ya jumla katika kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki, litakuwa ni jukumu la Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya:

i. kuingiza masuala ya kukabiliana na maafa katika mipango ya Wilaya;

ii. kufuatilia majanga, vihatarishi vinavyosababisha majanga na matishio ya maafa na hali za jamii zilizo katika hatari ya kukumbwa na maafa katika Wilaya;

iii. kufanya tathmini za kujua uwezekano wa kuathiriwa na maafa katika maeneo ndani ya Wilaya na kushauri njia muafaka za kupunguza uwezekano huo;

iv. kuratibu utekelezaji wa kazi za kukabiliana na maafaza taasisi mbali mbali na kutafuta fedha na rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kukabiliana na maafa;

v. kusaidia na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na maafa iliyokubaliwa na Kamisheni kwa Wilaya;

vi. kuhakikisha kwamba kazi za kukabiliana na maafa za Wilaya zinalingana na vipaumbele na miongozo ya Serikali;

vii. kuandaa tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kusimamia programu za mafunzo na kujenga uwelewa kwa jamii;

viii. kuanzisha vikundi na mfumo wa kujihami wa kiraia wa maafa katika Wilaya;

ix. kuhakikisha kunaanzishwa kwa vyombo vya kujiandaa na kujihami na maafa katika ngazi ya Wilaya na Shehia; na

x. kutekeleza maamuzi yoyote yaliyotolewa na Kamisheni.

Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

16. Kunaanzishwa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya katika kila Wilaya, Zanzibar.

Muundo wa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya

17. (1) Kunaanzishwa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya katika kila Wilaya, Zanzibar.

(2) Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Baraza la Mji au Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya.(2) Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) afisa sheria wa Serikali ya Mtaa;

(b) maafisa wa Sekta wa Serikali za Mitaa;

(c) mwakilishi wa Chama cha Msalaba Mwekundu wa Wilaya;

(d) mwakilishi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi wa Wilaya;

(e) mwakilishi wa Kikosi cha Valantia Zanzibar wa Wilaya;

(f) mwakilishi wa Idara ya Uhamiaji;

(g) afisa anayehusika na kukabiliana na maafa Wilaya;

(h) afisa mipango wa Wilaya; na

(i) wajumbe watatu wanaoteuliwa na Mkuu wa Wilaya kutoka katika taasisi zisizo za Serikali na Jumuiya za kijamii zinazohusika na masuala ya kukabiliana na maafa baada ya kushauriana na taasisi husika ndani ya Wilaya.

(3) Afisa Mipango wa Manispaa au Halmashuri ya Wilaya atakuwa Katibu wa Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

Kazi za Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya

18. (1) Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na jukumu la kutekeleza maamuzi ya Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya kuhusu mambo ya kukabiliana na maafa katika eneo la Wilaya.

(2) Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya itakuwa na jukumu la kuishauri Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya kuhusu mambo yote ya kukabiliana na maafa.

Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia

19. Kunaanzishwa katika kila Shehia Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia.

Muundo wa Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia.

20.(1) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia itakuwa chini ya uenyekiti wa Sheha.

(2) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) wajumbe wa Baraza la Ushauri la Shehia;

(b) wawakilishi wawili wa Jumuiya za kiraia ndani ya Shehia;

(c) mwakilishi wa Watu wenye Ulemavu; na

(d) Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wa Majimbo na Wadi husika.

(3) Katibu wa Shehia atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Kukabiliana na Mafaa ya Shehia.

Kazi za Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia.

21. Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuandaa mipango na taratibu za kukabiliana na maafa katika meneo yao;

(b) kusimamia matukio ya maafa na dharura ili kutoa misaada inayohitajika kwa familia zilizoathirika;

(c) kutafuta fedha na rasilimali zinazohitajika kwa ajili kukabililiana na maafa;

(d) kuainisha majanga katika maeneo husika na kufanya uchambuzi wa viashiria vya maafa;

(e) kuanzisha vikundi vya kiraia vya kukabiliana na maafa;

(f) kujenga uwezo na kusimamia kazi za kukabiliana na maafa katika ngazi ya familia; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote itakayoelekezwa na Kamisheni.

Vikao vya Kamati.

22. (1) Kamati zitafanya vikaovyake vya kawaida kila robo mwaka.

(2) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti na asipokuwepo, Wajumbe watachagua Mjumbe miongoni mwao kuendesha kikao hicho.

(3) Kamati itaweka na kuhifadhi kumbukumbu za vikao na kumbukumbu hizo zitathibitishwa katika kikao kinachofuata na zitasainiwa na Mwenyekiti.

Maamuzi ya Kamati

23. Maamuzi ya Kamati yataamuliwa kwamakubaliano, iwapo wajumbe wameshindwa kufikia makubaliano, katika maamuzi yoyote maamuzi yataamuliwa kwa kura; na iwapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya ziada ikijumuisha kura yake ya awali.

Akidi ya Vikao

24. (1) Akidi ya Vikao vya Kamati katika vikao vya kawaida, itakuwa zaidi ya nusu ya Wajumbe wote.

(2) Katika tukio la dharura, kuwepo kwa angalau Wajumbe watano wa Kamati kutawezesha akidi.

(3) Kamati zinaweza kutayarisha kanuni za vikao vyao.

(4) Kamati zinaweza kumualika mtu yeyote kushiriki kwa jambo maalum katika vikao vya Kamati, isipokuwa mtu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

SEHEMU YA NNE
MIPANGO YA KUPUNGUZA NA KUKABILIANA NA MAAFA

Mpango wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar

25. (1) Mkurugenzi Mtendaji ataandaa Mpango Kukabiliana namaafa Zanzibar ambao utathibitishwa na Kamisheni.

(2) Mpango wa Kukabiliana na maafawa Zanzibar utajumuisha yafuatayo:

(a) kupunguza athari za maafa, kujiandaa, kukabili na kurudisha hali baada ya maafa kutokea;

(b) matukio maalum kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) majukumu na wajibu wa vyombo vinavyohusika;

(d) vipaumbele vya kupunguza na kukabiliana na maafa kwa visiwa vyote vya Zanzibar ikijumuisha na eneo lake la bahari;

(e) mpangilio wa kutoa misaada kutoka katika Mataifa na mashirika ya misadaa;

(f) masuala ya utoaji wa misaada na utaribu wa Kamati ya Maafa ya Wilaya; na

(g) jambo jengine lolote linalohitajika.

Mipango ya Kukabiliana na maafaya Wilaya

26. (1) Afisa anayehusika na kukabiliana na maafa wa Wilaya ataandaa Mpango wa Kukabiliana na Maafa wa Wilaya ambaoutathibitishwa na Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya.

(2) Mpango wa Kukabiliana na Maafa wa Wilaya utajumuisha yafuatayo:

(a) Kupunguza athari za maafa, kujiandaa, kukabili na kurudisha hali baada ya maafa kutokea;

(b) matukio maalum yatakayotokea katika Wilaya;

(c) majukumu na wajibu wa vyombo vinavyohusika;

(d) vipaumbele vya kupunguza na kukabiliana na maafa katika Wilaya; na

(e) jambo jengine lolote linalohitajika.

Mipango ya Kisekta ya Kukabiliana na maafa

27. Kila Wizara, Idara au Wakala itaandaaMpango wa Kisekta wa Kukabiliana na Maafa unaoendana na Mpango wa Kukabiliana na Maafa wa Zanzibar.

Miongozo

28. Kamisheni kupitia Mkurugenzi Mtendaji inaweza kutayarisha na kutoa miongozo ya maandishi kwa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Wilaya, Wizara, Idara na Wakala kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Kukabiliana na Maafa pamoja na mambo mengine yoyote yanayohitajika.

SEHEMU YA TANO
NGAZI ZA MAAFA, TAMKO NA MAWASILIANO

Ngazi za Maafa

29. (1) Maafa yatakuwa katika ngazi ya jamii ikiwa:

(a) yataathiri Shehia moja au Wilaya moja na eneo lake;

(b) mipango na taratibu ziliyopo katika Wilaya au Shehia zinatosheleza kukabiliana na maafa; na

(c) mazingira mengine yoyote yatakayoonesha haja ya kutangaza maafa katika ngazi ya jamii kamaitakavyotangazwa na Mkuu wa Wilaya.

(2) Maafa yatakuwa katika ngazi ya kitaifa ikiwa:

(a) yameathiri zaidi jamii na kusababisha upotevu wa maisha na au maradhi, madhara kwa watu na upotevu wa mali; na

(b) mazingira mengine yoyote yakayoonesha haja ya kutangaza maafa katika ngazi ya jamii kama itakavyotangazwa na Rais.

Kutangaza hali ya Maafa katika ngazi ya Wilaya na Shehia

30. Endapo Kamati za Kukabiliana na Maafaza Shehia na au Wilaya zitaridhishwa kwamba hali ya maafaimezidi uwezo wao, Mkuu wa Wilaya kwa kushauriana na Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika na kuthibitishwa na Kamisheni, atatangaza hali ya maafa kwa Shehia au Wilaya husika.

Kutangaza hali ya Maafa ya Kitaifa

31. (1) Endapo Kamisheni ikiridhika kuwa hali ya dharura na maafa iliyopo katika eneo lolote la Zanzibar, na ikiwa uwezo wa Serikali wa kukabiliana na maafa hayo umezidiwa, Mwenyekiti wa Kamisheni atamjuilisha Raisipasavyo.

(2) Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais anaweza kutangaza hali ya maafa iliyopo Zanzibar.

Kipindi cha Kutangaza hali ya Maafa ya Kitaifa

32. Tamko la Rais litatekelezwa kuanzia tarehe lilipotangazwa na litamalizika kwa kipindi kisichozidi miezi miwili na itakapoonekana kuna haja ya kuongezwa, tangazo hilo litatolewa tena kwa kipindi kisichozidi miezi miwili.

Mawasiliamo na utaratibu wa utoaji maelekezo

33. (1) Mwenyekiti waKamisheni anaweza kutoamaelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji kuhusu utekelezaji wa kazi zake.

(2) Kamisheni kupitia Mkurugenzi Mtendaji inaweza kutoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati ya Kukabiliana na maafa ya Wilaya.

(3) Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya kupitia Mwenyekiti inaweza kutoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa kazi za Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Shehia.

Upatikanaji wa Rasilimali wakati wa Maafa

34. (1) Endapo ikionekana naKamisheni na Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya kwamba:

(a) rasilimali inayomilikiwa na mtu yeyote ikihitajika kwa ajili ya kazi za kukabiliana na maafa;

(b) jengo au eneo lolote likihitajika kwa ajili ya kazi za uokozi; au

(c) chombo chochote cha usafiri wa barabarani, baharini au angani kilichosajiliwa Zanzibar kikihitaji kwa ajili ya matumizi ya usafiri wa kwenda au kutoka katika eneo la maafa au usafiri kwa ajili ya kazi za uokozi au kurejesha hali baada ya maafa,mamlaka hiyo itatumia rasilimali hizo au majengo kwa madhumuni ya kukabiliana na hali ya dharura na maafa.

(2) Iwapo rasilimali, eneo, jengo au vyombo vya usafiri wa barabarani, baharini au angani vitahitajika kwa mujibu wa Kifungu hiki, muda wa mahitaji hayo hautozidi muda wa tangazo la hali ya maafa lililotolewa na Rais.

(3) Katika Kifungu hiki, "rasilimali" inajumuisha nguvukazi, huduma, vifaa kama vile ghala, zana, vyombo vya usafiri na nyenzo.

Uwezo katika hali ya dharura au maafa

35. Wakati wa kipindi cha hali ya dharura na au maafa, Kamishenina au taasisi yoyote inayohusika inaweza kutumia uwezo wa dharura inapohitajika kwa ajili ya kukinga upotevu wa maisha ya watu, maradhi au madhara kwa watu au wanyama, upotevu au uharibifu wa mali au mazingira.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Kamisheni

36. (1) Kutakuwa na Akaunti Maalum ambayo itaingiza fedha zote za Kamisheni kama zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Kamisheni inaweza katika kutekeleza kazi zake na kwa mujibu wa masharti ya fedha hizo zilizopatikanwa, kutumia fedha hizo kwa malipo, posho, mishahara gharama za kazi na malipo yoyote muafaka yanayojitokeza ikijumuisha matumizi muhimu.

Vyanzo vya fedha

37. (1) Matumizi ya fedha yatafanywa na Mkurugenzi Mtendaji kwa idhini ya Kamisheni.

(2) Fedha na rasilimali za Kamishenizitatokana na:

(a) kiasi cha fedha kama kitakavyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku;

(b) michango, misaada na mikopo ambayoKamisheni inaweza kila baada ya muda kupokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(c) fedha nyengine zinazoweza kupatika na ama kutokana na utekelezaji wa majukumu yake au vyenginevyo.

Makadirio

38. (1) Mkurugenzi Mtendaji katika kila mwaka wa fedha husika, atawasilisha kwa Kamisheni mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Kamisheni kwa ajili ya mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa mapendekezo ya Kamisheni, bajeti ya Kamisheni itahusishwa katika sehemu ya makadirio ya bajeti ya Wizara husika.

Ukaguzi wa Hesabu

39. (1) Kamisheni itawezesha kuwekwa na kuhifadhiwa vitabu vya hesabu vinavyoainisha mapato na matumizi ya Kamisheni.

(2)Mkurugenzi Mtendaji, kwa mujibu wa maelekezo ya Kamisheni ataandaa katika mambo yanayohusiana na utekelezaji wa Kamisheni, taarifa ya fedha ya kila mwaka ambayo itajumuisha:

(a) ripoti ya fedha na taarifa ya mapato na matumizi; na

(b) taarifa nyengine yoyote inayohusiana na mambo ya fedha ya Kamisheni kama inavyohitajika na Sheria ya Fedha za Umma.

(3) Ndani ya kipindi cha miezi mitatu ya kufunga mwaka fedha, hesabu zikijumisha taarifa za fedha za Kamisheni kwa mwaka huo zitawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mfuko wa Kukabiliana na Maafa

40. (1) Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, kutakuwa na Mfuko wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar ambao utajumuisha:

(a) fedha zote zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika makadirio ya bajetiya mwaka;

(b) misaada iliyoidhinishwa na Serikali;

(c) michango ya wananchi;

(d) fedha nyengine zinazoweza kupatikana kutoka katika Mfuko Maalum utaoanzishwa na Serikali; na

(e) fedha nyengine yoyote zinazotokana na adhabu zilizoainishwa chini ya Sheria hii, fedha nyengine zozote ambazo zimewekwa au zimepatikana ama kutokana na utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

Malengo ya Mfuko

41. Mfuko utatumika kwa malengo yafuatayo:

(a) kutoa huduma za maafa;

(b) kazi za uokozi;

(c) misaada ya kibinadamu wakati wa dharura au maafa ya ngazi ya Kitaifa, Wilaya na Shehia;

(d) kukodi ardhi, vifaa, ununuzi wa vifaa na nyenzo nyengine na kuanzisha majengo ya dharura wakati wa maafa; na

(e) lengo jengine lolote kwa matumizi ya Mfuko ambalo Kamisheni inaona muhimu kwa kukabiliana na maafa.

SEHEMU YA SABA
MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu

42. (1) Mtu ambaye:

(a) amekataa kutekeleza majukumu yake bila ya sababu ya msingi;

(b) amefanya kitendo chochocte kisichoruhusiwa; au---

(c) amekataa kusalimisha mali zake au kutoa huduma wakati wa maafa,ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni moja na isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Mbili au Kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

(2) Mtu ambaye atamzuia mtu aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tano na isiyozidi Shilingi za Kitanzania MilioniMoja au Kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

Makosa yanayohusu kukataa kutoa Taarifa

43. Mtu ambaye amekataa kutoa taarifa yoyote inayohitajika na Kamisheniinayohusiana na maafa, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Mbili na isiyozidi Shilingi za Kitanzania Laki Tano au Kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote mbili.

Makosa yanayohusiana na kutoa tahadhari za uongo.

44. Mtu ambaye anatoa tahadhari au taarifa za uongo ambazo zitasababisha usumbufu au hasara kwa watu ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Mbili na isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Tatu au Kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI MENGINEYO

Kulindwa kwa kitendo kilichofanywa kwa nia njema

45. Hakutakuwa nashtaka lolote kwa afisa wa Kamisheni kwa kitendo chochotealichokifanya kwa nia njema katika kutekeleza majukumu yakealiyopewa afisa huyo kwa mujibu wa Sheria hii.

Ripoti ya Maafa

46. Kwa madhumuni ya kukusanya taarifa sahihi za maafa, mtu yeyote ambaye atasimamia au atafanya kazi za maafa atawasilisha ripotikwaKamisheni.

Kanuni.

47. Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii, bila ya kuathiri masharti ya jumla, Waziri anaweza kutunga Kanuni katika mambo yafuatayo:

(a) kusimamia utekelezaji mzuri wa majukumu ya Kamisheni;

(b) kusimamia kazi za ziada za Kamati;

(c) kuidhinisha upatikanaji au umiliki wa vyombo vya usafiri wa barabarani, baharini na mali nyenginezo;

(d) kuainisha vituo vya utekelezaji kazi za Kamati kabla, wakati na baada ya maafa;

(e) kuendeleza Mpango wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar;

(f) usimamizi bora wa Mfuko wa Kukabiliana na Maafa Zanzibar; na

(g) mambo mengine yoyote yanayohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

MADHUMUNI YA MSWADA WA SHERIA

Madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria mpya inayoweka mfumo wa kisheria katika shughuli za kukabiliana na mada ambayo itaondosha mapungufu yanayoonekana katika sheria ya sasa.

Aidha, sheria mpya itawiana na Sera ya kukabiliana na Maafa ya mwaka 2011 pamoja na makubaliano na mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya kukabiliana na maafa iliyoridhiwa na nchi yetu. Yote haya yanafanyika kwa lengo la kupunguza athari za vifo, mali na mazingira kwa kuchukua hatua za kujikinga, kujitayarisha kukabiliana na kurudisha hali baada ya dharura au maafa.

Mswada huu umegawika katika sehemu vinane

Sehemu ya Kwanza: inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina fupi la Sheria, kuanza kutumika kwake pamoja na tafsiri za misamiati inayotumika katika Mswada.

Sehemu ya Pili: inaelezea kuhusu kuundwa kwa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Wajumbe wa Kamisheni, Kazi za Kamisheni, Uwezo wa Kamisheni, Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, Kuanzishwa kwa Sekretariati ya Kamisheni, Vitengo vya Kamisheni na kazi za Sekretarieti.

Sehemu ya Tatu: inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Kamati za kukabiliana na Maafa kati ka ngazi ya Taifa, Wajumbe wa kila Kamati na majukumu ya Kamati hizo pamoja na kuelezea utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Kamati hizo.

Sehemu ya Nne: inaelezea kuhusu utayarishaji wa Mipango ya kukabiliana na Maafa katika ngazi za Taifa, Wilaya na Sekta pamoja na utaratibu wa kutoa miongozo kuhusu utayarishaji wa Mipango hiyo.

Sehemu ya Tano: inatoa maelezo kuhusu ngazi za maafa (classification) na utaratibu wa kutangaza hali ya maafa katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia. Aidha sehemu hii pia, inaelezea utaratibu wa kutoa maagizo katika masuala ya kukabiliana na maafa, upatikanaji wa nyenzo za kukabiliana na maafa wakati wa maafa na uwezo wa Kamisheni na Taasisi nyengine wakati wa dharura na maafa.

Sehemu ya Sita: inaelezea masuala ya bajeti na upatikanaji wa fedha na matumizi ya Kamisheni, ukaguzi wa hesabu na suala la uanzishwaji Mfuko wa Kukabiliana na Maafa pamoja na madhumuni yake.

Sehemu ya Saba: inahusu makosa na adhabu ikiwemo makosa yanayohusu kukataa kutekeleza majukumu bila sababu ya msingi, kufanya kitendo kisichoruhusiwa kinachohusiana na masuala na maafa, kukataa kutoa taarifa, kukataa kusamilisha mali na kutoa huduma wakati wa maafa na kutoa tahadhari za uongo.

Sehemu ya Nane: inahusu masharti mengineyo yanayoelezea kuhusu kinga ya Afisa wa Kamisheni, utoaji wa taarifa za maafa, uwezo wa Waziri Kutunga Kanuni, kufuatana na kubakiza Sheria ya Kukabiliana na Maafa Namba 2 ya Mwaka 2003.

.....
(Mohamed Aboud Mohamed)
WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS